

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA UKEREWE**  
**MKOA WA MWANZA.**

Simu+255 282 515 056 /+255 685 304 646

Email: [ps@ukerewedc.go.tz](mailto:ps@ukerewedc.go.tz)

Tovuti: [www.ukerewedc.go.tz](http://www.ukerewedc.go.tz)



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),  
S.L.P. 41,  
NANSIO/UKEREWE.

*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb. Na. GA.25/95/01/107

01/06/2022

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya wilaya ya Ukerewe anawatangazia nafasi za kazi nne (04) tu za **Dereva Daraja la II**, kwa watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kazi hii .Tangazo hili ni kutokana na kibali cha Ajira chenye **kumb Na .FA.97/228/01/9** cha Tarehe 13 Mei 2022. Kutoka kwa **Katibu mkuu ofisi ya Rais menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.**

**1.0 DEREVA II NAFASI NNE(04)**

**1.1 SIFA ZA MWOMBAJI**

- I. Awe mtanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45
- II. Awe amehitimu na kufauru kidato cha nne.
- III. Awe na leseni ya Dereva daraja E au C1 ya uendeshaji magari ambayo ameifanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajari.

- IV. Awe amehudhuria mafunzo ya Msingi ya uendeshaji Magari (**Basic driving course**) yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliw na serikali. Waombaji wenye cheti cha majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

## 2.0 MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbali mbali kwenye safari za kikazi.
- iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
- iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbali mbali.
- v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
- vi. Kufanya usafi wa gari
- vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake.

## 3.0 MASHARTI YA KAZI

Ajira ya kudumu (Permanent Terms)

## 4.0 MSHAHARA

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia viwango vya Serikali yaani **TGS - B1**

## 5.0 MASHARTI YA JUMLA

- i. Maombi yote yatumwe na nakala za vyeti vya taaluma, cheti cha kuzaliwa pamoja na kitambulisho cha NIDA au namba ya NIDA, nakala za vyeti vithibitishwe na mahakama au mwanasheria alieidhinishwa au kutambulika na serikali.
- ii. Testimonials, Provisional results, Statement of Results, Hati za matokeo ya kidato cha nne na sita **HAVITAKUBALIWA**.
- iii. Waombaji wote waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe kuwa Vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika ya NACTE au NECTA.
- iv. Watumishi wote waliowahi kufanya kazi katika utumishi wa umma wakaacha kazi, kustaafu, wakastaafishwa au kufukuzwa kazi hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali cha Katibu Mkuu Utumishi.
- v. Vyeti vyote vitafanyiwa uhakiki kwa kushirikiana na mamlaka husika NECTA na NACTE.



- vi. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na.CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 novemba 2010.
- vii. Mwombaji aambatanishe picha mbili za Rangi (passport size) za hivi karibuni.
- viii. Maombi yaambatishwe na maelezo binafsi (CV).
- ix. Maombi yatakayoletwa moja kwa moja bila kupitia posta hayatafanyiwa kazi.
- x. Mwisho wa kutuma Maombi ni Tarehe 14 Juni 2022 saa 9: 30 Alasiri. Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta tu kupitia Anwani:-

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),  
HALMASHAURI YA WILAYA YA UKEREWE,  
S.L.P 41,  
NANSIO/UKEREWE.**



.....  
Emmanuel .L. Sherembi  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
NANSIO/UKEREWE**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
UKEREWE**

